



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF WATER  
BUKOPA WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY

Kitekele Road, P. O. BOX 81, Bukoba,  
Tel: +255 (0) 282221744 Fax: 0282221588  
Email: info@buwasa.go.tz Website: www.buwasa.go.tz



In reply please quote:

Ref No. BUWASA/MJ/C.44/35

18/01/2022


Permanent Secretary,  
Ministry of Water,  
Government City,  
Maji Street,  
P.O BOX 456,  
DODOMA.



**REF: REQUEST FOR PAYMENTS TSH 376,191,052.20 OF KARABAGAIN WATER PROJECT UNDER COVID – 19 FUNDS.**

Refer the heading above.

2. The Authority entered into contracts with suppliers and Local Fundi for the above mentioned water project. Therefore, we received requests for the same worth Tshs **376,191,052.20** (Three hundred million seventy six one hundred ninety one thousand fifty Two and twenty Cents) as a final payment for implementation of this Project.
3. With this regard, the Authority is submitting and requesting payments for the same as per attachment.
4. Ongoing project report has been Attached.

  
Eng. Matage Dotto  
Ag. Managing director  
BUWASA

BOARD MEMBERS

Mr. Samora F.A. Lyukurwa - Chairman  
Municipal Director - Member  
Mrs. Editha N. Mugurubi - Member  
Mrs. Monica G. Kishu - Member  
Jafari A. Athuman - Member

RAS - Kagera - Member  
Mrs. Mary G. Karega - Member  
Mrs. Kagemulo C. Lupenka - Member  
Hon. Shaban Said - Member  
Mr John N Siraz - Secretary



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF WATER  
BUKOPA WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY

Kitekele Road, P. O. BOX 81, Bukoba,  
Tel: +255 (0) 282221744 Fax: 0282221588  
Email: info@buwasa.go.tz Website: www.buwasa.go.tz



PAYMENT REQUESTS FOR IMPEMENTATION OF KARABAGAIN WATER SUPPLY PROJECT UNDER COVID-19 FUNDS

SNO	AWARDED CONTRACTOR/SUPPLIER	DESCRIPTION OF CONTRACT	CONTRACT NUMBER	CONTRACT AMOUNT	PAYMENT AMOUNT DUE	INVOICE NO
1	Fundi Imani Mussa	Construction of Sump of 50m3	AE/031/2021-2022/W/02 Lot-01	6,900,000.00	6,900,000.00	Local fundi
2	Fundi Domisian Bagezi	Construction of Raiser Tank of 135m3	AE/031/2021-2022/W/02 Lot-03	18,412,220.00	18,412,220.00	Local fundi
3	Fundi Antony Bahebe	Construction of Pump House and Toilet	AE/031/2021-2022/W/02 Lot-02	3,340,000.00	3,340,000.00	Local fundi
4	Fundi Nelson	Construction of domestic point and fusing	AE/031/2021-2022/W/02 Lot-04	43,222,000.00	43,222,000.00	Local fundi
5	Magereza-Bukoba	Excavation of Trench and backfilling	AE/031/20212022/W/08	48,375,000.00	48,375,000.00	Local fundi
6	Ndekagi Tanzania Limited	Supply of Local Material	AE/031/2021-2022/G/68Lot-1	30,644,600.00	15,050,009.20	0179

7.	Joytrix Company Limited	Supply of Round bars and Paints	AE/031/2021-2022/G/68Lot-3	34,137,000	2,435,000.00	029
8	Joytrix Company Limited	Supply of Cement and Blocs Materials	AE/031/2021-2022/G/68Lot-2	71,208,500.00	44,058,500.00	034
9	Hassaratan Genera Supply	Supply of fittings	AE/031/2021-2022/G/66	24,617,160.00	6,707,500.00	125
10	PLASCO	Supply of HDPE pipes	AE/031/2021-2022/G/67	253,925,055.92	150,633,507.00	1741
11	ADELINA P. KITALE	Supply of building material	AE/031/2021-2022/G/68 Lot 2	9,937,000	9,937,000	1776 & 1777
12	Supply of water Pump with H=110m and Q=52m <sup>3</sup> /hr	Supply and Install of surface pump	AE/031/2021-2022/G/68 Lot 5	27,120,316.	27,120,316	0056
	Total amount requested				<b>376,191,052.20</b>	

Regards



Eng. Matage Dotto

Ag. Managing Director

**BUWASA.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI  
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA  
Barabara ya Kitekele, S.L.P 81, Bukoba,  
Simu: +255 (0) 282221744 Faksi: 0282221588  
Barua pepe: info@buwasa.go.tz Tovuti: www.buwasa.go.tz



Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na BUWASA/MJ/C.44/36

17/01/2022

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Maji,  
Mji wa Serikali,  
Mtaa wa Maji,  
S.L.P 456,  
Dodoma.

**YAH: KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAJI KATA YA  
KARABAGAINI.**

Rejea somo tajwa hapo juu.

2. Naomba kuwasilisha taarifa fupi ya hali ya utekelezaji wa mradi wa Maji kata ya Karabagaine. Taarifa hii imejikita kujua nini kimepagwa kufanyika kwa mradi mzima, mpango wa utelezaji kwa awamu hii kwanza kwa mfuko wa Fedha za COVID-19, gharama za mradi mzima na matumizi ya fedha za Covid katika mradi huu.
3. Pia kupitia taarifa hii nimekuelezea hatua tuliyofikia kwa sasa na taarifa za fedha kutoka wizara ya fedha.
4. Hivyo kupitia taarifa hii nakuhakikishia kuwa tutakamilisha mradi huu kwa wakati na matumaini yetu makubwa ni pesa zitaendelea kutolewa kwa wakati ili kutokwama kwa utekelezaji huu wa mradi.
5. Wako katika utekelezaji

  
Inj. Matage Dotto

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

**BUWASA.**

## Table of Contents

1.0 UTANGULIZI .....	3
2.0 UJENZI WA MRADI YA KARABAGAINI( <i>COVID 19-FUND</i> ) .....	3
3. HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KARABAGAINI.....	4
4. HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA.....	5
5. HITIMISHO.....	5

## **1.0 UTANGULIZI**

Mamlaka ya maji na usafi wa Mazingira Bukoba(Buwasa) inatekeleza Sera ya serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. Ambapo malengo ya Serikali ni kufikia asilimia 85% kwa wananchi waishio vijijini na asilimia 100% kwa wananchi waishio Mjini ifikapo Desemba, 2022. Mradi wa maji Karabagaine umesanifiwa na wataalamu wa Mamlaka ya maji Bukoba ili kuweza kupunguza kero kubwa ya Maji kata ya karabagaine. Kata ya karabagaine ina jumuisha vijiji vitano ambavyo ni Kitwe, Itahwa, Kiziru, Kangabusharo na Ibraizibu. Pia mradi huu unategemea kuongeza uzalishaji kata ya Kagondo. Mradi huu unategemea kuhudumia idadi ya watu wapatao 16,104 kwa mwaka 2022, hata hivyo mradi utaweza kuendelea kuhudumia wateja wapatao 25,877 ifikapo mwaka 2043. Kwa maana hiyo Mradi wa maji utapokea maji kutoka tanki la Magoti lenye Ujazo wa 1,200,000 na tunategemea kuzalisha maji lita 1,155,000 kwa siku yatayosukumwa kwenda Kata ya Karabagaine.

Mradi huu unategemewa kujengwa Tanki kubwa (02) ujazo wa 225m<sup>3</sup> chini ya Ardhi, ujazo wa tanki 135m<sup>3</sup> juu ya mnara wa mita sita, Maunganisho ya wateja wapatao 200, ujenzi wa vituo, viosiki(ghati), ulazaji wa bomba 43.78km. Kiasi cha Tsh 1,871,081,851.89 kinategemewa kukamilisha mradi huu na kuweza kutatua changamoto ya maji kata ya karabagaine na Kagondo.

Hivyo kulingana na maelekezo ya Mh raisi ya kuwasilisha mapendekezo ya miradi inayoweza kujenga kwa haraka na kunusuru maeneo ya Changamoto za maji. Ofisi ilipokea maelekezo na kuwasilisha andiko la ujenzi wa miradi isiyozidi kiasi cha Tsh 550,000,000. Tuliwasilisha mradi huu wa Karabagaine na kuamua kuujenga kwa awamu mbili. Awamu hii itahusisha upelekeaji wa maji kwa vijiji vya Kiziru, Itahwa na Kitwe na kiasi cha pesa 550,000,000 Kitaweza kukamilisha kazi hii.

## **2.0 UJENZI WA MRADI YA KARABAGaine(COVID 19-FUND)**

Mradi wa Maji Karabagaine kwa maelekezo ya fedha za Covid-19 tunategemea kupokea pesa kiasi cha Tsh 550,000,000 ziweze kujenga mradi huu. Hadi sasa ofisi bado haijapokea kiasi cha pesa toka wizarani. Mradi huu kwa upande kwa COVID-19 kazi zinazotegemewa kufanyika ni kwa vijiji vya Kiziru, Itahwa na Kitwe kazi hizo ni kama ifuatavyo;

- (i) Ujenzi wa Nyumba ndogo ya kupokelea maji( *sump well*) yenye ukubwa wa lita 50,000, Nyumba ya Mitambo(Pump house) pamoja na choo. Majengo haya yatajengwa eneo la Itahwa

- (ii) Ujenzi wa tanki kubwa la kuhifadhi maji ukubwa wa lita 135,000 juu ya mnara wa mita sita(6m) ene la kiziru
- (iii) Ufungaji wa pampu yenye uwezo wa kuzalisha lita 1,150,000 kwa siku
- (iv) Ujenzi wa maghati(06) na DP(06) ambavyo vitajengwa DP(02) na Magati(02) kwa kila kijiji cha kitwe, Itahwa na Kiziru kwa kuzingatia maeneo yaliyopendekezwa na viongozi wa vijiji
- (v) Ulazaji wa bomba kuu la kupeleka maji 3km kwenye eneo lililopendekezwa kujengwa tanki.
- (vi) Ulazaji wa bomba za usambazaji 16.35km kwa vijiji hivyo vitakavyonufaika kwa kipindi cha fedha za CoviD-19
- (vii) Usimikaji wa vigingi, ujenzi wa chemba na ujenzi wa fensi maeneo ya sump na tanki
- (viii) Ufungaji wa umeme eneo la nyumba ya mitambo.

Kwa kazi hizo zilizoordheshwa ndio zitagemewa kukamilika kwa kipindi kisichozidi miezi 06 kama maelekezo yalivyotolewa na viongozi, hivyo makadirio ya pesa Tsh 550,00,000 yatatoshwa utekelezaji wa mradi. Baada ya awamu hii kukamilika ofisi itaendelea kuomba fedha kuweza kupeleka maji kwa vijiji vilivyosalia kama Ibaraizibu, Kagondo na Kangabusharo.

### **3. HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KARABAGAINI**

Mradi tushaanza hatua za awali za utekelezaji ikiwa hatua za usanifu na upembuzi imekamilika na uwasilishaji wa taarifa

#### **➤ UJENZI WA TANKI LA MAJI UJAZO WA LITA 135,000 MNARA WA 6M**

Ujenzi wa tanki la Mnara wa tanki umeendelea hadi kufikia sasa mnara wenye urefu wa mita 6 kati ya sita umejengwa. Kazi ya ujenzi iko 56.78% ya kazi yote. Vifaa vya ujenzi vinaendelea kupokelewa hadi kufikia na ujenzi unajengwa kwa kasi na matumaini yetu kufikia mwezi february 30, kazi itakuwa imekamilika

#### **➤ UJENZI WA NYUMBA YA MITAMBO**

Ujenzi wa nyumba ya mitambo unaendelea na tunaendelea na hatua ya kufunga mbao kwa ajili ya kupaua. Hivyo ujenzi wa nyumba hii ya mitambo uko 78% ya kazi yote na tunategemea kukamilisha mwisho mwa mwezi huu january.

➤ **UJENZI WA TANKI DOGO LA KUPOKELEA MAJI SUMP TANK UJAZO WA 50,000 LITA**

Ujenzi wa tanki dogo la kupokela maji hadi sasa umefikia 77.4% ya kazi zote ujenzi wa kuta umekamilika za kubeba maji, tunaendelea na hatua za ujenzi wa mfuniko wa tanki(top slab) na kupiga lipu za tanki hilo. Kazi inategemewa kukamilika kabla ya tarehe 10.02.2021

➤ **UJENZI WA VITUO VYA KUCHOTEA MAJI**

Mradi huu tunategemea kujenga vituo(DP) sita na Magati/Virula vitatu. Hadi kufikia sasa tumejenga virula vitatu na ujenzi wa Vituo vitano kati ya sita umekamilika hadi kufikia sasa

➤ **ULAZAJI WA BOMBA**

Tunategemea kulaza bomba urefu wa 19.5km kwa mradi mzima, hadi kufikia sasa hakuna kazi iliyofanyika tunategemea kupokea bomba ili tuendelea na kazi.

Kwa ufupisho hali ya utekelezaji wa Mnara huu wa Karabagaine iko wastani wa 50% hadi kufikia sasa, na tunategemea kumaliza kazi hii mapema mwezi wa tatu, Matumain yetu makubwa kuwa pesa zitatufikia kwa wakati ili tuweze kumaliza kazi hii.


**4. HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA**

Kama taarifa inavyoeleza kwa Awamu hii ya kwanza kiasi cha Tsh **550,000,000** kimetengwa kwa Ajili ya ujenzi wa Mradi huu kwa Awamu hii ya Kwanza. Hadi kufikia sasa kiasi cha Tsh 178,182,225,34 tu kimepokelewa na kiasi cha Tsh **155,643,217.61** tayari kimeshatumika kulipa wazabuni, tunaendelea kumaliza hatua za kulipa Tanesco kiasi cha Tsh **24,156,172.12**. Kupitia taarifa hii tumewasilisha kwako Maombi ya Tsh **376,191,052.20** kwa ajili ya kumaliza kazi iliyobaki kwenye Mrad huu

**5. HITIMISHO**

Hivyo tunamatumaini makubwa kuwa pesa ziataendeelea mapema iwezekanavyo. ofisi ya Mkurugenzi mtendaji inategemea kukamilisha mradi kabla ya wakati uliopangwa kwa ajili ya utekelezaji huu. Mradi huu tunategemea kukamilisha kwa kutoa huduma ndani ya mwezi wa nne mwaka huu. Nawasilisha taarifa hii fupi kuweza kupata kiasi cha pesa ili kumaliza kazi hii.

Wako katika utekelezaji



Inj. Matage Dotto

Kaimu Mkurugenzi mtendaji

**BUWASA**